GRPS my choice®
Grand Rapids Public Schools

# MWONGOZO WA COVID-19

**Mpendwa Mzazi/Mlezi (Walezi),**

Tunafurahia kuwapa Mwongozo wetu wa GRPS wa COVID-19.

Mwongozo huu unanuia kuwa marejeleo ya haraka kwa wazazi na walezi wote wa GRPS tunapoendelea kupambana na janga la COVID-19.

Hii ni hati ya kudumu ambayo itasasishwa wakati mabadiliko au maelezo mapya yanapotolewa.

Ikiwa una maswali au unahitaji maelezo zaidi, tafadhali wasiliana na shule.

Mwaminifu,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule


02 **Matarajio ya Usalama wa Afya ya Wafanyakazi na Wanafunzi**

03 **Dashibodi ya Data ya COVID-19**

04 **Kikumbusho cha Dalili ya Mwanafunzi**

05 **Hatua ya Kuchukua ikiwa Mtoto Ametambuliwa kuwa na Ugonjwa/Watu Waliokaribiana na Mgonjwa**

06 **Mchoro wa Utaratibu wa Huduma Maalum ya Barakoa katika Wilaya**

07 **Utaratibu wa Usafi**

08 **Usafiri**

09 **Kusasisha Maelezo ya Mawasiliano**

# MATARAJIO YA USALAMA WA AFYA YA WAFANYAKAZI NA MWANAFUNZI YA COVID-19

Wapendwa Wanafunzi, Wazazi, Walezi na Wafanyakazi,

Kwanza kabisa, asanteni kwa kujitolea kwenu kuendelea na ustahimilivu katika nyakati hizi zenye sintofahamu zinazobadilika kila uchao.

Ninaandika kurudia matarajio ya afya ya wafanyakazi na wanafunzi wetu.

1. **Unapaswa kuvaa barakoa kila wakati kwenye majengo ya wilaya ya GRPS.**
2. **Unapaswa kukaa nyumbani ikiwa unahisi yoyote kati ya dalili hizi dalili bila kujali hali ya chanjo:**

   - Homa ya 100.4F AU kuhisi joto unapoguswa
   - Kukohoa kusiko kwa kawaida au kubadilika kikohozi
   - Kushindwa kupumua
   - Kupoteza hisia ya kuonja au kunusa kusiko kwa kawaida
   - Maumivu ya koo
   - Maumivu ya mwili
   - Kuharisha, kutapika au kichefuchefu
   - Maumivu makali ya kichwa
   - Kuchoka sana
   - Kufungana kwa pua ua kutokwa makamasi

   **Pia kaa nyumbani ikiwa hujachanjwa NA:**
   - Umekaribiana au kuishi na mtu ambaye ametambuliwa kuwa na COVID-19
   - Unaishi na mtu ambaye ana dalili za COVID-19 na anasubiri matokeo ya vipimo
3. **Hatua za usalama wa afya ukiwa kwenye majengo:** Ikiwezekana, tafadhali kaa umbali wa futi 6 na uvalie barakoa ipasavyo zinazofunika pua na mdomo wako KILA WAKATI. Nawa mikono ipasavyo na udumishe usafi wa mkondo hewa.

Tungependa kila mtu awe salama na mwenye afya, kwa hivyo sharti tuwe waangalifu kwa hatua tunazochukua. Asante.

Mwaminifu,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule

# DASHIBODI YA VIPIMO VYA COVID-19

| KIPIMO | LENGO | LENGO KIWANGO CHA HATARI UFAFANUZI | VYANZO VYA DATA |
|---|---|---|---|
| **KIWANGO CHA MAAMBUKIZI KATIKA KAUNTI**<br>*Wastani wa siku 7* | **chini ya asilimia 5 HATARI NDOGO**<br>Zingatia asilimia 5 hadi 10 | **VIWANGO VYA HATARI**<br>Chini = chini ya asilimia 5<br>Wastani = asilimia 5 hadi 8<br>Juu zaidi = asilimia 8 hadi 10<br>Juu kabisa = zaidi ya asilimia 10 | Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent |
| **TUKIO LA KAUNTI KATI YA 100,000**<br>*zaidi ya siku 7* | **Lenga chini ya visa 9 kwa watu elfu 100**<br>Zingatia zaidi ya visa 10 kati ya watu elfu 100 | **VISA KATI YA WATU 100,000:**<br>Chini = chini ya 9<br>Wastani = 10 hadi 49<br>Juu zaidi = 50-99<br>Juu kabisa = zaidi ya 100 | Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent<br>Kituo cha Kudhibiti Ugonjwa |
| **KIWANGO CHA CHANJO YA KAUNTI**<br>*Wastani wa siku 7* | **LENGA zaidi ya asilimia 70** | **Asilimia (%) ya idadi ya watu wanaotimiza masharti waliopokea chanjo zote mbili*** | Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent |
| **MISIMBO YA POSTA YA GRPS KIWANGO CHA CHANJO**<br>*Wastani wa siku 7* | **LENGA zaidi ya asilimia 70** | **Asilimia (%) ya idadi ya watu wanaotimiza masharti waliopokea chanjo zote mbili*** | Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent |

Dashibodi ya Takwimu ya GRPS ya COVID-19 itajazwa na data na kusasishwa kila wiki kwenye tovuti ya wilaya. Dashibodi ya Data itatumiwa kuongoza hatua ya uamuzi ya Wilaya yetu kupitia ushauri wa Idara ya Afya ya Kaunti ya Kent.

*Waliopokea chanjo kamili = angalau wiki 2 zimepita tangu dozi ya pili ya chanjo ya dozi 2 (Pfizer/Moderna), au chanjo ya dozi moja (Johnson & Johnson)

# COVID-19 MWANAFUNZI DALILI KIKUMBUSHO

**Kabla uondoke shuleni tafadhali mchunguze mwanafunzi wako ikiwa ana dalili za COVID-19.**

**Mtoto wako akae nyumbani ikiwa anahisi yoyote kati ya dalili hizi bila kujali hali ya chanjo:**

- Homa ya F 100.4 au zaidi AU joto anapoguswa
- Kukohoa kusiko kwa kawaida au kubadilika kwa kikohozi
- Kushindwa kupumua
- Kupoteza hisia ya kuonja au kunusa isiyo ya kawaida
- Maumivu ya koo
- Maumivu ya mwili
- Kuharisha, kutapika au kichefuchefu
- Maumivu makali ya kichwa
- Uchovu kupita kiasi
- Msongamano au makamasi puani

**Pia mtoto wako asalie nyumbani ikiwa hajachanjwa NA:**

- Amekaribiana au kuishi na mtu ambaye ametambuliwa kuwa na COVID-19.
- Mwanafunzi au mwanafamilia yeyote anayesubiri matokeo ya vipimo vya COVID-19.

**Ikiwa unaamini kuwa dalili za mwanafunzi wako zinahusiana na ugonjwa tofauti, tafadhali wasiliana na mwuguzi wa shule kabla mtoto wako aende shuleni.** Unaweza kuhitaji kutoa ithibati ya utambuzi huu.

Mtoto wako akihisi dalili zifuatazo siku za shule, shule itamtenga na wengine na kukupigia upangie jinsi ya kumchukua. Tukishindwa kuwasiliana nawe, tutapiga simu kwa namba za dharura kwenye Synergy. Ni muhimu sana uhakikishe kuwa umesasisha maelezo yako ya mawasiliano katika Synergy.

# COVID-19

## Unachopaswa kufanya ikiwa Mwanafunzi Atatambuliwa Kuwa Mgonjwa au Amewekwa Karantini

Wilaya itafuata Masharti na utaratibu wa MDHHS/OSHA ikiwa mtu ametambuliwa kuwa na COVID-19, ikiwa ni pamoja nakutokana na kuripoti na masharti ya kuhifadhi rekodi. Wilaya itakusanya maelezo ya mawasiliano ya watu wote waliokaribiana na mgonjwa kuanzia siku mbili kablaaonyeshe dalili hadi wakati ambapo alikuwa shuleni mara ya mwisho.

**Ikiwa una dalili zinazohusiana na COVID-19 bila kujali hali ya chanjo unapaswa:**

**01** Kukaa nyumbani

**02** Kujulisha shule yako

**Ukija shuleni na uhisi dalili siku za shule, unapaswa:**

**01** Kujulisha mwalimu/mwuguzi wa shule

**02** Kuondoka shuleni mara moja

Ukitambuliwa kuwa na ugonjwa au kuwekwa karantini kwa sababu ya kumkaribia aliyeambukizwa:

**01** Kaa nyumbani au uondoke shuleni mara moja.

**02** Wasiliana na mwuguzi wa shule. Mwuguzi wako wa shule atafuatilia watu waliokaribiana na mgonjwa na atakupa miongozo ya kujitenga/karantini.

Kukaribiana na mgonjwa ni kuwa ndani ya futi 6 kwa dakika 15 au zaidi katika kipindi cha saa 24.

# COVID-19 MCHAKATO WA BARAKOA

Kwa mujibu wa Kituo cha Kudhibiti Magonjwa (CDC), Miongozo ya Jimbo la Michigan na Office of Civil Rights (OCR), wanafunzi, wafanyakazi na wageni wote wanapaswa kuvaa barakoa katika majengo yote ya wilaya. CDC na OCR inadokeza kwamba, hata hivyo, sehemu ndogo ya watu kwa sababu ya ulemavu au hali ya matibabu iliyoandikwa inaweza kukosa kuvaa barakoa au haiwezi kuvaa mask kwa usalama kwa sababu ya hali hizi zilizoandikwa. Watu wanaotimiza masharti ya mojawapo ya vikundi hivi kwa sababu hawawezi kuvaa barakoa kwa mujibu wa mwongozo wa CDC hawapaswi kuvaa.

Hata hivyo, ikiwa mwanafunzi mwenye ulemavu hawezi kuvaa barakoa, kukaa mbali na wengine, au kuzingatia masharti mengine ya afya ya umma, mwanafunzi huyo bado ana haki ya FAPE. Iwe wanahudhuria masomo ya mahali walipo au ya ana kwa ana, wanafunzi ambao hawawezi kuvaa barakoa kwa sababu ya ulemavu wao hawapaswi kunyimwa huduma au kuadhibiwa kwa kutotimiza masharti ya barakoa na sharti waendelee kufunzwa bila kubaguliwa.

Huduma maalum zinaweza kuwa pamoja na lakini sio tu:

- Kifunika uso
- Aina Mbalimbali ya Barakoa/Miundo
- Vigawanyaji Maalum
- Kubadilisha Ratiba
- Mapumziko ya Mara kwa Mara
- Motisha
- Ukubwa wa Darasa
- Sahihi/Thabiti Barakoa na Nyingine PPE kwa Wengine Wanaohudumia au Kusoma Pamoja na Mwanafunzi

* **Masomo ya mahali ulipo yanaweza kuzingatiwa ikiwa hakuna huduma yoyote maalum iliyofanikiwa na kwa wanafunzi wenye ulemavu, ofa yao ya elimu ya umaa inayofaa bila malipo inaweza kutimizwa kikamilifu.**

Kwa maombi ya **mwanafunzi** kutovalia barakoa, tafadhali wasiliana na mwuguzi wa shule.

Kwa maombi ya Mfanyakazi kutovalia barakoa, tafadhali wasiliana na Idara ya **Wafanyakazi** kupitia HumanResources@grps.org.

## CHATI YA KUTOVALIA BARAKOA YA WILAYA

**Mwanafunzi na mfanyakazi, kwa sababu ya ulemavu au hali ya matibabu iliyoandikwa, hawawezi kuvaa barakoa au hawatakuwa salaama kwa kuvaa barakoa kwa sasa.**

Kagua Data na Ubaini Msingi wa Ustahimilivu

Kagua Data na Ubaini Huduma ya (za) Msingi ya Kuimarisha Ustahililivu na KUFUNZA Kuvaa Barakoa

Kagua Data Kila Wiki kwa Ongezeko la Ustahimilivu katika Mazingira

Tekeleza Huduma Maalum

Kagua Data katika Vipindi vya Wiki 3 ili Kubaini Mapendekezo Zaidi

**NYENZO:**
http://bit.ly/covid-19-civil-rights-Q-and-A

# COVID-19 USAFISHAJI VIKUMBUSHO

## UFAFANUZI

**Usafishaji** huondoa viini na uchafu kwenye sehemu au vifaa kwa kutumia maji na sabuni. Hatua hii haiangamizi viini lakini hupunguza kiwango cha hatari ya kusambaa kwa maambukizi.

**Kutakasa** hupunguza idadi ya viini kwenye sehemu au kifaa kwa kiwango kinachokubalika, kwa mujibu wa viwango vya afya ya umma na hupunguza hatari ya kusambaa kwa maambukizi.

**Kuua viini** huangamizi viini kwenye sehemu au vifaa kwa kutumia kemikali lakini haisafishi sehemu chafu. Tunapendekeza kuwa usafishe sehemu na vifaa kwa kutumia sabuni na maji kabla ya kuua viini.

## Tunaipa kipaumble afya ya wanafunzi na wafanyakazi wetu.

Kuvaa barakoa, kunawa mikono na kukaa mbali na watu wengine kadri iwezekanavyo itakuwa muhimu kuwa na shule salama.

Usafishaji hupunguza kiwango cha hatari kwa kuondoa na kuangamiza viini kwenye sehemu zinazoguswa mara kwa mara. Shule yako ina utaratibu wa kusafisha majengo.

Bidhaa za usafishaji zinazotumiwa zinatimiza viwango vinavyopendekezwa vya CDC, EPA na sera za wilaya.

- Shule husafishwa kila usiku.
- Ratiba ya usafishaji wa majengo mara kwa mara au wakati wowote inapohitajika.
- Hatua ya kuzuia kushiriki vifaa kwa pamoja zinatumika.
- Mabafu ya pamoja na sehemu za kutumiwa na watu wengi husafishwa mara kwa mara siku za shule.

# COVID-19 USAFIRI WA BASI TAARIFA

**NAMBARI MPYA YA DHARURA YA USAFIRI**
**(616) 819-6100**

## USAFIRI WA BASI LA MANJANO MIONGOZO YA USALAMA WA AFYA:

- Unapaswa kuvaa barakoa
- Wanafunzi wa Chekechea na darasa la 1 watapangwa
- Viti viwili vya kwanza katika sehemu zote mbili za basi hazitakaliwa
- Abiria wote wanapaswa kukaa mbali na wenzao
- Ndugu wanaweza kukaa pamoja

# COVID-19 MAELEZO YA MAWASILIANO TAARIFA

Mpendwa Mzazi/Mlezi (Walezi),

Kutokana na kubadilika kwa hali mara kwa mara na uamuzi unaohusiana na COVID na shule zetu, ni muhimu sana wilaya na shule ziwe na maelezo ya mawasiliano yaliyosasishwa na idhini ya wazazi na walezi.

Wazazi na walezi sharti waidhinishe wilaya na shule kutuma barua pepe, simu za kiotomatiki, na ujumbe. Wazazi na walezi wanaweza kufikia fomu za idhini kupitia akaunti ya ParentVue. Utahitaji nambari ya mwanafunzi ya mtoto wako ili kujaza fomu ya idhini, ambayo inapatikana pia kwenye ParentVue.

Tunahimiza wazazi na walezi wajiandikishe ili kupokea mawasiliano hayo.

Ili ujaze fomu ya idhini ya mtandaoni, tembelea https://bit.ly/grps-contact-consents-form.

Tunahimiza wazazi na walezi waweke alama ya kupendezwa kwenye kurasa za Facebook ya wilaya na shule maalum na kufuatilia tovuti ya wilaya kupitia grps.org ili kupata maelezo na habari muhimu.

Ikiwa una maswali yoyote wasiliana na shule ya mwanafunzi wako. Asante!

Mwaminifu,

Leadriane Roby, Ph.D.
Msimamizi wa Shule